

## Sheria ya READ ni nini?

Sheria ya READ ni sheria ya Colorado inayoweka miongozo ili kuhakikisha kuwa kila mwanafunzi anakamilisha daraja la tatu la kusoma kwenye au juu ya kiwango cha daraja. Inasaidia shule kutambua wanafunzi wanaohitaji msaada wa mafunzo ili kusoma kwenye kiwango cha daraja

## Ni nini maana ya “kusoma zaidi chini ya kiwango cha daraja”?

Hii inamaanisha kuwa mwanafunzi anasoma mwaka mmoja au zaidi chini ya kiwango chake daraja la sasa. Utafiti unaonyesha kuwa kusoma kwenye kiwango cha daraja kufikia mwisho wa mwaka wa shule ni muhimu kwa ufanisi wa shule wa baadaye.

## Mpango wa READ ni nini?

Mpango wa READ ni mpango wa kuchukua hatua ya mtu binafsi kwa chekechea kupitia wanafunzi wa daraja la 3 waliotambuliwa kama wenye matokeo ya chini sana ya kiwango cha daraja katika kusoma. Mpango unaendelea hadi mwanafunzi afikie ufasaha wa kiwango cha daraja katika kusoma.

Mpango wa READ umeundwa ili kumsaidia mtoto wako kujiendeleza kama msomaji mwenye:

- \* **Malengo mahususi ya kusoma**
- \* **Msaada wa mafunzo ya shule**
- \* **Msaada wa nyumbani**



Shule za Umma za Aurora  
Kitengo cha Usawa katika Masomo  
Aurora, Colorado 80011  
15001 E 1st Ave.

## Sheria ya READ:

Taarifa za Familia



*Kushirikisha shule na familia ili kuhakikisha ufanisi wa mwanafunzi katika kusoma*

## Ni Taarifa zipi muhimu zaidi?

Lengo letu katika Aurora Public Schools ni kwa watoto WOTE kuhitimu kutoka shule ya upili wakiwa tayari kwa elimu ya baadaye au kwa utendakazi. Kuwaandaa wanafunzi kwa hili kunaanza pindi tu wanapoingia shuleni.

### Tathmini

Mwalimu wa mtoto wako hutumia Tathmini ya Kuendeleza Usomaji (DRA2) ili kutambua kiwango cha kusoma cha kila mwanafunzi.

Taarifa hii ya tathmini inaonyesha kuwa mtoto wako anasoma chini ya kiwango cha daraja.

Ikiwa mtoto wako ni Mwanafunzi wa Lugha ya Kiingereza, alama za tathmini ya lugha ya jimbo (ACCESS) zinatoa taarifa kuhusu maendeleo ya mtoto ya lugha ya Kiingereza. Viwango vya kusoma na maendeleo ya lugha vinazingatiwa ndani ya Mpango wa READ kwa Wanafunzi wa Lugha ya Kiingereza.

### *Mpango wa READ umeundwa ili kusaidia ukuaji wa binafsi wa mtoto wako katika kusoma.*

### Misaada ya Shule

Mwalimu wa mtoto wako na wafanyakazi wengine wa shuleni hufanya kazi pamoja ili kuteua mikakati na hatua zinazotimiza malengo ya Mpango wa READ wa mtoto wako.

Hili halihusu hatua tu. Timu pia inatafuta njia kufanya mafunzo ya darasani kufikiwa na wanafunzi wote.

### Misaada ya nyumbani

Watu wazima walio nyumbani ni washirika muhimu wa kuwasaidia wanafunzi kuwa wasomaji, waandishi na watu bora kwa mawasiliano.

Tafadhali shirikiana na mwalimu wa mtoto wako ili kuunda na kutekeleza mpango wa READ.

### Makongamano na mazungumzo ya mwisho wa mwaka kuhusu kusalia shuleni

Kila mwanafunzi mwenye Mpango wa READ atakuwa na kongamano la mwisho wa mwaka ili kukagua na kufanya kazi pamoja kujiandaa kwa mwaka unaofuata.

Wakati wa kongamano, mwalimu wa mtoto wako atashiriki machaguo yanayohusiana na mahitaji mahususi ya mtoto wako.

Watoto wengine huenda wakahitaji zaidi ya mwaka mmoja ili kuelewa. Sheria inasema kuwa kusalia shuleni linaweza kuwa chaguo, lakini kuna njia na misaada mingine mingi. Utafiti unaonyesha kuwa kurudia kiwango cha daraja huenda lisiwe chaguo bora mara nyingi.

Wanafunzi wa Lugha ya Kiingereza (ELLs): Mikakati bora ya maelekezo kwa mafunzo ya lugha na kusoma na kuandika inaamuliwa kwa usaidizi kutoka kwa mwalimu ambaye ni mtaalamu wa mafunzo ya lugha ya Kiingereza. Sheria ya jimbo la Colorado haitoi pendekezo la kusalia shuleni kwa wanafunzi ambao wanaendelea vizuri katika Kiingereza kama lugha yao ya pili au nyingine.



## Ni vipi ninavyoweza kumsaidia mtoto wangu nyumbani?

*Haya hapa ni baadhi ya mawazo. Mwalimu wa mtoto wako pia anayashiriki.*

Mfanye mtoto wako afahamu kuwa **ufanisi wa shule ni muhimu** kwako.

Hakikisha kuwa mtoto wako **anakuja shuleni** kila siku.

*Sikiliza, zungumza, soma na uandike kwa lugha yako ya nyumbani. Kuendeleza ujuzi huu kwa lugha yako ya nyumbani kutamsaidia mtoto wako kusoma na kufikiria.*

**Mazungumzo** ni muhimu. Ongea kuhusu:

- Siku yake shuleni
- Vitabu anavyosoma
- Hali ambazo mmeshiriki pamoja
- Hadithi za familia/hadithi nyingine zinazofahamika

**Msomee** na msome na mtoto wako kila siku.

- Soma vitabu vinavyofahamika anavyofurahia.
- Sikiliza vitabu kwenye mkanda/CD, kompyuta, au Vitabu vya mtandaoni.
- Ongea kuhusu anachosoma. Nini kilichotendeka? Alijifunza nini?

**Andika** na mtoto wako kila mara. Mawazo mengine ni pamoja na: Barua kwa familia au marafiki, orodha za ununuzi, hadithi au habari za majarida.

**Fanya mazoezi ya ujuzi wa maneno.** Tumia herufi za plastiki au sumaku ili kupanga, mpangilio wa ABC, linganisha herufi kubwa na ndogo, unda maneno rahisi, na utamke majina ya jamii.